# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA AFYA

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
**Simu: 0734005777 Barua Pepe:hlpc@afya**

## TANGAZO

**MAOMBI YA USAJILI**

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu wahitimu wote wa astashahada, stashahada na shahada ya Maabara ya Afya kuwa dirisha la usajili liko wazi, hivyo wahitimu wote wanasisitizwa yafuatayo;

1. Wahitimu ambao hawana usajili wa awali au wa kudumu wanasisitizwa kufanya maombi kabla ya dirisha kufungwa tarehe 30.01. 2025.
2. Aidha, Waliofanya mtihani wa usajili kabla ya mfumo kuanza (Kabla ya Machi 2023) wawasiliane na ofisini msajili 0734005777 Kabla ya 30.01.2025 baada ya hapo watalazimika kuanza uataratibu mpya wa kufanya mitihani
3. Mwombaji wa usajili lazima ambaatanishe nyaraka zifuatazo ili maombi yake yafanyiwe kazi kwa wakati.
    - Cheti cha kuzaliwa
    - Cheti cha elimu ya sekondari
    - Barua ya utambulisho kutoka chuo alichohitimu
    - Cheti cha matokeo ya chuo (Transcript)
    - Cheti cha taaluma cha chuo (Kwa waombaji wa usajili wa kudumu)
    - Cheti cha uthibitisho (Recognition of award) kutoka TCU (Kwa wahitimu waliosoma vyuo vya nje ya nchi)
4. Maombi haya yanafanyika kwa njia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz.*** Waombaji wote wanasistizwa kutunza jina tambuzi (username/email) pamoja na nywila (password) zilizotumika wakati kufungua akaunti kwenye mfumo wa HPRS muda wote kwani akaunti hiyo itatumika kwa kipindi chote.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na:
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
24.12.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
24 DEC 2024
P.O.Box 743
DODOMA

***"Heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya"***